# MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

*Na.19. Msimu wa Kilimo 2022/23* *Tathmini ya Machi 21-31, 2023 na Matazamio kwa Kipindi cha Aprili 1-10, 2023*



**MUHTASARI**

- Wakulima katika maeneo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka, wanashauriwa kumalizia shughuli za kupanda mazao husussan yale yanayokoma haraka na kustahimili ukame wakifuata ushauri wa maafisa ugani
- Kwa ujumla zao la mahindi katika maeneo yanayopata mvua za Msimu yapo katika hali ya kuridhisha.
- Wakulima, wafugaji na wavuvi wanahimizwa kuzingatia taarifa za hali ya hewa kwa shughuli na mipango ya kila siku.



## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31, 2023

Katika dekadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliimarika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azores na Siberia) ilipungua nguvu kidogo. Hali hii ilipelekea ukanda mvua (ITCZ) kusukumwa kuelekea kaskazini na hivyo kuwepo katika maeneo ya kaskazini mwa Tanzania.

Joto la bahari katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi lilikuwa la juu kidogo hususan katika maeneo ya kaskazini mwa Madagascar. Hali hii ilisababisha kutokea kwa migandamizo midogo ya hewa iliyosaidia kuimarisha ukanda mvua. Hali kadhalika, mfumo wa Wimbi Anga (MJO) uliendelea kuimarika na hivyo kuendelea kusababisha vipindi vya mvua na ngurumo kwa baadhi ya maeneo nchini.

## TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31, 2023

Katika dikadi hii, maeneo mengi ya nchi yalipata mvua ya zaidi ya milimita 11. Hata hivyo, maeneo machache ya mkoa wa Rukwa, Katavi, Tabora na Lindi yalipata mvua zaidi ya milimita 200 kama inavyoonekana katika kielelezo.




Kielelezo: Kiasi cha mvua katika kipindi cha Machi 21-31, 2023

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31, 2023

Mvua zilizonyesha katika dikadi hii zimeongeza unyevunyevu katika udongo ambao umesaidia ukuaji na mendeleo ya mazao.
Kwa ujumla mahindi katika maeneo yanayopata mvua za Msimu yapo katika hatua ya kubeba kwa mkoa wa Njombe na katika hatua ya kukomaa kwa mikoa ya Mbeya, Ruvuma, Rukwa, Iringa, Tabora, na Kigoma. Aidha, mahindi katika maeneo yanayopata mvua za Msimu yapo katika hali ya kuridhisha.

Zao la mpunga lipo katika hatua ya ukuaji katika maeneo ya kusini mwa Morogoro, na mikoa ya Tabora, Mbeya, na Rukwa.
Kwa upande wa maeneo yanayopata misimu miwili ya

mvua kwa mwaka, wakulima wameendelea kupanda mazao kwa ajili ya msimu wa Masika.
Zao la viazi mviringo lipo katika katika hatua ya kukomaa katika mikoa ya Iringa, Njombe na Mbeya na baadhi ya wakulima wameendelea kuvuna zao hilo.
Upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo na wanyamapori ulikuwa wa kuridhisha katika maeneo mengi nchini kutokana na mvua zinazoendelea.

## HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA MACHI 21-31, 2023

Kwa ujumla kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito na mabonde viliendelea kuongezeka kutokana na mvua zilizonyesha.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 1-10, 2023

Katika dekadi hii, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia inatarajiwa kuongezeka nguvu kidogo wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia inatarajiwa kupungua nguvu. Hali hii inatarajiwa kuendelea kuusukuma Ukanda Mvua (ITCZ) kuelekea kaskazini mwa nchi hususan katika maeneo yanayopata misimu miwili ya mvua kwa mwaka.
Joto la bahari katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi linatarajiwa kuwa la juu kidogo hususan katika maeneo ya kaskazini mwa Madagascar na hivyo kusababisha uwepo wa migandamizo midogo ya hewa.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 1-10, 2023

Maeneo ya kanda ya Ziwa Viktoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara), nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa), magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora), pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) pamoja na pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba) yanatarajiwa kuwa na mvua na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo.

Maeneo ya kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa mkoa wa Morogoro) na nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) yanatarajiwa kuwa na mvua na ngurumo za radi katika maeneo machache.

## HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA APRILI 1-10, 2023

Mvua zinazotarajiwa katika maeneo mengi nchini zitaongeza unyevunyevu kwenye udongo ambao utaendelea kusaidia ukuaji na maendeleo ya mazao.
Wakulima katika maeneo yanayopata mvua za Msimu wanashauriwa kuendelea kufuatilia kwa ukaribu maendeleo ya mazao mashambani na milipuko ya wadudu waharibifu na magonjwa ya mimea kwa kufuata ushauri wa maafisa ugani.

Wakulima katika maeneo yanayopata mvua mara mbili kwa mwaka, wanashauriwa kumalizia shughuli za kupanda mazao hususan yale yanayokoma haraka na kustahimili ukame wakifuata ushauri wa maafisa ugani juu ya mbegu na aina za mazao yanastahili kupandwa kwa kipindi hiki.

Wavuvi wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku, za kwenye maziwa makuu na baharini ili kufanya maamuzi juu ya wakati sahihi wa kwenda kufanya shughuli za uvuvi.

Jamii inashauriwa kuzingatia utabiri wa hali ya hewa kwa shughuli na mipango yao ya kila siku.

## HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA APRILI 1-10, 2023

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito kinatarajiwa kuongezeka kidogo kutokana na mvua zinazotarajiwa. Hata hivyo, jamii inashauriwa kuvuna maji ya mvua kwa ajili ya matumizi ya baadae.



Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo Kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz; agromet@meteo.go.tz; Tovuti: *www.meteo.go.tz*
(ISO 9001:2015 Certified in Aviation Services)